# GREDI 8; KISWAHILI SIMPLIFIED NOTES

## CBC RATIONALIZED WORK

*Well-organized, simplified learning notes that provide clear, concise information in a logical sequence, making key concepts easily accessible and memorable, enhancing understanding and retention while fostering engagement and facilitating effective study.*

*By providing a clear focus on key ideas, these Mwalimu Consultancy Notes foster better retention and comprehension, making learning more accessible and enjoyable.*

**UPDATED VERSION**


This is a Free Sample/Overview of the Original Notes

*CONTACT US FOR COMPLETE VERSION OF THE NOTES*



***Mr Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000***

**MWALIMU CONSULTANCY**

# SARUFI

Ni utaratibu wa sheria zinazotawala matumizi sahihi ya muundo wa lugha.sheria hizi za lugha ndizo huleta ufasaha na usanifu katika luhga na kumwezesha mzungumzaji kuelewa tungo zinazotolewa na mzungumzaji. Kila lugha huwa na sheria zake katika utunzi wa maneno.

## AINA ZA MANENO

kuna aina nane za maneno katika lugha ya Kiswahili. Hizi ni

a. vivumishi
b. viwakilishi
c. nomino
d. vielezi
e. vihusishi
f. vihisishi
g. viunganishi
h. vitenzi

## NOMINO

Ni aina ya maneno inayotaja majina ya watu, mahali , kitu , au hali. Ili sentensi iwe kamili lazima nomino au kiwakilishi chake kitumiwe. Kuna aina saba za nomino , hizi ni:

*Nomino za pekee/ maalum*

Hizi ni nomino halisi zinazotaja majina ya watu, mahali, siku au miezi vitu na Mungu

Nomino hizi zinapo andikwa ,hutangulizw kwa herufi kubwa.nomino hizi ni:

Nomino zinazotaja mahali: Kenya, Tanzania , Eldoret Kisumu, Mlima Kenya, Mto Nyiro .n.k

Nomino zinazotaja siku : Jumapil, Jumanne n.k

Nomino zinazotaja sikukuu: Siku ya Madaraka, Krisimasi, Iddi Mubarak n.k Nomino zinazotaja majina ya watu: Faith, Adul, Jelimo, Nafula. Otieno. Nk Nomino zinazotaja miezi: Agosti, January , Oktoba.

Nomino zinazotaja dini: Kiyahudi Kiiislamu , Kikristo.

Nomino zinazotaja luhga na lahaja: Kingereza , Kiamu, Kiarabu Kijaluo.

## NOMINO ZA KAWAIDA

Nomino hizi hutaja vitu vya kawaida visivyo vya kipekee, havina ubainifu wowote.sio lazima ziwe na herufi kubwa katika maandishi kama vile zilivyo nomino za pekee.nomino hizi zinaweza kuwa na umoja na wingi, hata hivyo kuna baahdi ya nomino za kawaida ambazo zina umoja au wingi tu.

Kwa mfano:

mwalimu/ walimu
kiti/viti
mtu/watu
redio (haina wingi)

## NOMINO ZA DHAHANIA

Ni majina ambayo hufikiriwa tu , hayawezi kugusika , kuonekana, kunusika wala kusikika. Mara nyingi huanza kwa kiambishi ‘U’ ingawa zingine zinaweza kuanza kwa herufi tofauti. Nomino hizi huwa katika fikra au akilini ma mtu.

Kwa mfano : ujinga, wivu , urembo, unono, woga ,wema , chuki mawaidha, utukufu mapenzi.

***NOMINO ZA JAMII/ MAKUNDI***

Haya ni majina ambayo hutaja vitu vilivyo katika vikundi, ni nomino ambazo ndani yake kuna vitu vingi. Hufumbata maana ya jumuiya ambayo inasifa yakauli moja.

Kwa mfano : Baraza la mawaziri, halaiki ya watoto ,, umati wa watu.

***NOMINO ZA KITENZI JINA/ KITENZI***

Ni majina ambayo huundwa kutokana na kitenzi. Hutambulishwa na kiambishi ‘KU’

Kwa mfano kucheza , kuimba , kusoma, kuchunguza.

***NOMINO ZA WINGI***

Ni nomino ambazo hutokea kwa wingi. Nomino hizi ni za kawaida ila tu hutokea kwa wingi pekee.

Kwa mfano:marashi, matata, marashi , mate , maji , machozi, matumizi, maringo,maudhui.

***NOMINO AMBATA/AMBATANI.***

Ni majina ambayo huundwa kutokana na maneno mawili mbalimabli Kwa mfano :

mpiga+ picha= mpigapicha

kinasa+sauti= kinasa sauti.

**VIVUMISHI**

Ni neon linalo eleza zaidi kuhusu nomino huvumisha nomino au majina. Kuna aina mbali mbali za vivumishi

***VYA SIFA :*** ni vivumishi vinavyoeleza sifa za nomino, jinsi gani illivyo. Vivumishi hivi hubadilika kutegemea ngeli za majina, yaani huchukuwa upatanisho wa kisarufi. K.m

-zuri( dada mzuri, ndizi nzuri)

-baya( mtu mbaya, kitu kibaya)

-tamu( chakula kitamu, maneno matamu)

***VYA IDADI*** : vivumishi hivi hufafanua jumla ya vitu vinavyohesabika au visivyohesabika. Vivumishi hivi huchukuwa viambishi kutegemea ngeli inayo husika.

Kwa mfano:

--ili ( watu wawili, mawe mawili, runinga mbili)

-haba( miti haba, watu haba , runinga haba)

-chache( miti michache, watu wachache, , runinga chache)

-ingi( watu wengi, miti nyingi, runinga nyingi)

## VIVUMISHI VIONYESHI/ VIASHIRAI

Huonyesha umbali au ukaribu wa nomino. Vivumishi hivi ni kama huyu, hawa, wale, hao, hivi . hapa .pale, mle.

***Vivumishi vionyeshi visisitizi***

Hutilia mkazo swala , jambo , nomino au jambo Fulani linalorejelewa kwa mfano: pale pale, kukohuko, mumo mumo, uu huu uo huo, uleule.

***Vivumishi vya pekee***

Vivumishi hivihuchukuwaa viambishi vya ngeli husika.

-*enye :* hutumika kuonyesha kuwa nomino Fulani inamiliki kitu Fulani k.m

mawe yenye rangi,

watu wenye miraba minne.

-*enyewe:* husisitiza nomino inayorejelewa.

**Kwa mafano**

mtoto mwenyewe alienda,

kiti chenyewe kilivunjika.

-*ote :* huonyesha ujumla wa vitu, watu au kitu pasipo na kubakisha. Kwa mfano wageni wote wamewasili,

mawe yote yali tumika.

*0-0te :* huonyesha dhna ya bila ubaguzi'. Hutumiwa kumaanisha kila' Kwa mfano : wageni wowote watawasili.

Mawe yoyote yatatumika

-*ingine:* hurejelea hali ya kuwa ' tofauti au 'zaidi ya kitu 'au mahali fulani. Kwa mfano :

Amenunua lori lingine

Kuchapa kwingine kunatisha.

-*ingineo*: hutumiwa kumaanisha badala ya[ au tofauti na' kitu kingine. Pia hutumika kama hitimisho ya orodha ambayo haikukamilika.

**Kwa mfano:**

Watu wengineo hapa ni wabaya

Bakuli linginelo nila mtoto.

## VIVUMISHI VIMILIKISHI

Vivumishi hivi huonyesha kitu Fulani kinamilikiwa na nomino fulani. Kwa mfano

Kiti chake

Redio yangu.

Vivumishi hivi hubadilika kiumbo kutegemea ngeli za nomino zinazotumika.

## VIVUMISHI VIULIZI

Huuliza swali kuhusiana na nomino inayohusika.

Kwa mfano : kiuulizi gani hakichukui kiambishi chochote na hutumika katika nominoya ngeli zote.

Kiulizi –pi huambishwa kiambishi kwenye nomina ya ngeli.

Kiulizi –ngapi vile vile huambishwa kiambishi lakini huuliza idadi ya nomino katika wingi pekee vivumishi nomino/ vivumishi vya jina kwa jina.

Hivi ni vivumishi vinavyo tumia nomino au majina kuvumisha nomino nyingine. Huchukuwa nafasi ya kivumishi katika sentensi ambapo huvumisha nomino nyingine.

**Kwa mfano**

Dada askari aligombea kiti cha eneo bunge.

Mwanasiasa zeruzeru anazifa nzuri.

Vivumishi vya a- unganifu: vivumishi hivi huundwa kwa mzizi wa kihusishi-a unganifu'. Vivumishi hivi hufananua daraja , umilikaji, au aina ya nomino husika. A, unganifu ina nafasi mbalilmbali katika sentensi kutegemea jinsi imetumika.

**Kwa mfano**

Mtoto wa dada amewasili--- umilikaji

Gaidi wa alshabab ni yule – kitambulizi/ aina.

Vivumishi rejeshi ni vivumishi vinavyo onyesha urejelezi wa nomino. Matumizi ya –ye na- o- ya urejeshi.

**Kwa mfano**

Mbuzi waliokufa watatupwa.

Gaidi aliyeshikwa atashtakiwa.

**VITENZI (T)**

Ni viarifa au maneno yanayotumiwa kuonyesha vitendo vinavyofanywa.vitenzi huwa na maana mbalimbali kulingana mnyambuliko wake. Kuna ina mbalimbali za vitenzi

**VITENZI HALISI**

Vi vitenzi vinavyo elezea matukio yanayofanyika, yatakayofanyika, yaliyofanyika, yatakayofanyika kwa nomino au jina k.m kulia kucheza kuimba. Vitenzi halisi vinaweza kutumiwa zaidi ya moja katika sentensi.

Kwa mfano

Rais amewasili nchini.

Mama anawalisha mifugo wake.

Vitenzi vikuu

Ni aina ya vitenzi halisi. Huwa na ujumbe mkuu katika sentensi . Hutokea cha pili katika sentensi iwapo kuna vitenzi viwili katika sentensi.

kwa mfano

Askari wa jiji walikuwa wakiwachapa wachuuzi kiholela

***VITENZI VISAIDIZI TS***

Hutumika na vitenzi vikuu au halisi katika sentensi ilikukamilisha jambo. Hutokea cha kwanza katika sentensi na kufuatwa na kitenzi halisi au kikuu , ilikuonyesha wakati kama ujao, uliopita ambapo kitendo kimefanyika.

Kwa mfano

Wanamichezo watakuwa wakipewa fidia na serikali.

***Contact Mwalimu Consultancy 0746 222 000 / 0742 999 000 for Complete Notes.***

Mtoto alikuwa akicheza na paka.

***VITENZI SAMBAMBA***

Ni vitenzi vinavyotokea kwa pamoja katika sentensi ilikutoa ujumbee kamili. Vitenzi vikuu vikitoke pamoja na vitenzi visaidizi kwa mfulilizo basi huitwa vitenzi sambamba.

Kwa mfano

Mtoto alikuwa akicheza na paka.

Baba alikwisha tambua alikuwa mkaidi.

***VITENZI VISHIRIKISHI (S)***

Ni vitenzi vinavyohitaji vijalizo ilikukamilisha uarifa wao kimaana.vitenzi hivi huonyesha hali au tabia Fulani ya kitu au mtu isiyokuwepo. Vitenzi hivi huwa vya aina mbili

vishikishi vikamilifu

Huchukuwa viambishi vinavyowakilisha nafsi, ngeli, wakati, au hali timilifu k.m 'ngali'' kuwa'

Mifano

Mtama ule ungali nkwenye jua.

Wanafunzi wamekuwa na mitihani wiki hii.

***VITENZI VISHIRIKISHI VIPUNGUFU***

Vitenzi vya aina hii havichukui viambishi vya wakati au ujao, hata hivyo huchukuwa viambishi vya nafsi au nafsi. Hivi ni ni, si ndi-, u, na li

Mifano katika sentensi

Kaka yu mtanashati.

Yeye ni mefu

## VIWAKILISHI.

Ni maneno yanayowakilisha nomino katika miktadha mbali mbali. Hufanya kazi ya jina katika sentensi , pia huitw vibadala .kuna aina mbalimbali ya viwakilishi.

***VIWAKILISHI NAFSI HURU***

Ni vile vinavyotumiwa kuonyesha umoja nawingi wa nafsi tatu za viumbe hai katika ngeli ya A-WA

Mimi , wewe ,sisi, yeye,wao, nyinyi.

***VIWAKISHI NAFSI TEGEMEZI***

Ni viambishi ngeli vya A-WA vinavyoambatanishwa na vitenzi, huwakilisha nafsi ya tatu. K.m

Wa watimba, mimi nitaimba.

***VIWAKILISHI VIMILIKISHI***

Huonyesha umilikaji wa nomino.

Mifano

Wangu ameenda

Wetu amewasili

***VIWAKILISHI VIULIZI***

Haya ni maswali yanayo wakilisha nomino.

Kwa mfano

Nani amefariki?

Wapi ni pake?

Ni yupi aliye na dosari?

Viwakilishi vya idadi

Hutaja idadi ya nomino.

Mifano

Wengi wameenda

Mmoja ni wake.

Wachache wataadhibiwa.

***VIWALKISHI VIONYESHI***

Husimamia nomino kuonyesha umbali au ukaribu uliko baina ya vitu viwili au zaidi.

Mifano

Yule ni mamake

Haya yatajadiliwa

Huo unatisha.

***VIWAKILISHI VISISITIZI.***

Mifano wawahawa ndio wezi waliotuingilia

Kilekile kimevunjika.

***VIWAKILISHI VYA 'A' UNGANIFU***

Huundwa kwa matumizi ya kihusishi -a- unganifu ilimkusimamia nomino. Mifano.

Wa sita amewasili( wakimbiaji)

Wa shamba( jogoo)

***VIWAKILISHI VYA SIFA***

Viwakilishi hivi huwakilisha tabia ya nomino .

Mifano

Mbaya aliuwawa( mzee)

Mrembo alitekwa nyara( binti)

**VIWAKILISHI VIREJESHI**

Hutokea pale ambapo amba- inasimama badala ya nomino

Mifano

Ambaye ameaga( fidel)

Ambayo haipendezi( chai)

**VIWAKILISHI VYA PEKEE**

Huchukuwa maumbo mbalimbali kutegemea jinsi inavyotumika. Kwa mfano -ote ( wote) wote waenda

-enye ( mwenye) mwenye kuiba ni Yule)

o-te( zenyewe) zenyewe zmeoza.

-ingine(jingine) jingine ndilo hillo.

-ingineo ( mengineo) mengineo yataliwa

## VIUNGANISI (U)

Ni neno au vifungu vya maneno vinavyo unganisha sentensi, virai au vishazi pamoja. Baadhi ya viunganishi ni kama na, au, lakini, kwa sababu, fauka ya , klicha ya, seuze ya, kwa maana n.k wanafunz i wataje baadhi.

**Mifano**

Licha ya Musa kuwa mwezi pia ni jambazi.

**VIHUSISHI**

Ni maneno yanayoonyesha uhusiano uliopo baina ya vitu, mahali watu au neon moja na jingine.

Vihusishi vya wakati kabla ya , tangu, hadi, baadaya.

Vihusishi vya mahali ndani ya , kando ya, chini ya, kati ya, ukingoni vihusishi mwa sababu kwa ajili ya, kwa vile kwa sababu ya n.k

**VIHISISHI( H.)**

ni maneno yanayo onyesha hisia za mzungumzaji.

Mifano Laiti! Lo! Oyee! Hoyee!

Zoezi

Tunga sentensi kwa kutumia vihisishi vifuatavyo

Maskini!, alhamdulullaih!, bu!, chubwi!

**VIELEZI(E**)

Ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi. Heleza jinsi kitendo kilivyo tendwa tendeka. Kuna aina mbalimbali ya vielezi

***VIELEZI VYA NAMNA/JINSI***

Hueleza namna au jinsi tendo lilitendeka . tendo lilitendeka aje. Mifano

Mkongwe alitembea poleole.

***VIELEZI VYA MAHALI***

Huonyesha au kueleza mahali tendo limetoka. Hueza jengwa kwa viambishi tamati –ni mifano alienda nyumbani, au kwa viambishi kama –po, -mo,-ko.

Mifano

Walimoingia wamejaa kunguru

Alikoenda nikucha

***VIELEZI VYA WAKATI***

hueleza wakati tendo linapofanyika. Huwa maneno kamili ya wakati usiku, jioni au vikadokezwa kwa kiambishi –po kilichoambishwa kwenye wa kitenzi.

Mifano

Alipowasili shimanzi ijijaa.

Tutahudhuria siku ya pili.

Alijifungua usiku.

***VIELEZI VYAA IDADI***

Hutaja kiasi ambacho kitendo kilifanywa, kitafanywa , huonyesha kitendo kimetendwa mara ngapi kwa mfano mara nyingi, tena, kila mwaka.

## MNYAMBULIKO WA VITENZI.

Ni hali ya kuongeza viambishi kwenye mzizi , haswa viambishi tamati na hivyo kukipa kitenzi kinacho husika maana tofauti. Kuna kauli mbalimbali za mnyambuliko

**Mfano**

Kauli ya kutenda

Huonyesha hali ya kutenda jambo., ambapo kiambishi ‘ a’ huongezwa kwenye mzizi .

**Kwa mfano**

Lima lima

Soma soma

Kauli ya kutendea

**Vitenzi vinavyoishia irabu - ‘ea’**

**Mifano**

Chora chorea

Sema semea

Vitenzi vinavyoishia irabu ‘ - i a’

**Mifano**

Finya finyia

Sifu sifia

Vitenzi vinavyoishia kwa –lea

**Mifano**

Ondoa ondolea

Bomoa bomolea

Vitenzi vinavyoishia kwa- lia

Pakua pakuwa
Fua fulia
Kaulika ya kutendwa
Kauli hii huonyesha athari kwa kitu kingine kwamba kitu Fulani kinapokea tendo fulani. Huwa na viambishi tamati au vimbishi hivi

Vinavyoishia kwa – wa
**Mifano**
Lipa lipwa
Kula kulwa

Vinavyoishia kwa – liwa au lewa
**Mifano**
Bomoa bomolewa
Chukuwa chukuliwa
Kauli ya kutendeka
Kauli hii huonyesha kutokea kwa jambo bila mhusika
Vitenzi vinavyoishia kwa vokali mbili –'aa; ua; ia huambishwa -'lika Mifano
Vaa valika
Tia tilika

Vitenzi vinavyo na irabu 'i u a' huchukuwa –'ika'
**Mifano**
Fahamu fahamika
pika pikika

Vitenzi vyenye vokali –e, o katika mzizi huishia kwa –eka
**Mifano**
Osha osheka
Cheza chezeka

Kauli ya kutendua
Huonyesha hali yakinyume, viambishi ni –'ua , oa.
**Mifano**
Kunja kunjua
Choma chomoa
Kauli ya kutendana
Ni hali ya kumtendea mtu jambo naye pia anakutendea, kitendo kinaenda pande mbili . kiambishi tamati ni –an'
**Mifano**
Soma someana
Tega tegeana

Kauli ya kutendata

Huashiriwa kwautumia kiambishi tamati –at' si maneno yote yanayoweza kunyambulika katika sehemu hii, kunabaadhi tu yameneno yanayoweza kunyambuliwa.

Mifano

Paka pakata

Fumba fumbata

Okoa okota

Kauli ya kutendama

Huonyesha kuwa kitenzi au kitendo kuwa katika hali Fulani bila kubadilika. Vitenzi vya aina hii havipatika kwa urahisi

**Mifano**

Lala lalama

Kwaa kwama

Ficha fichama

Kauli ya kutendesh

Mnyambuliko huu huchukuwa miundo tofauti tofauti.

Mifano

-esha

Cheza chezesha

Kishio –'za'

Tembea tembeza

Kishio-vya

Mlevya,

Kishio –'fya

Ogofya

Kishio –sha

Pikisha

# TANABAHI

Sio vitenzi vyote vya lugha ya Kiswahili huwa na sifa ambazo tumeziona hapo juu kunavitenzi vyenye asili ya kigeni na vyenye silabi moja. Katika kunyambua vitenzi vyenye silabi moja huambishwa 'KU mwanzoni iliviweze kueleweka.

Mfano kula , kupa, kunywa.

Katika Kiswahili kuna wakati ambapo muundo wa neno unaelekea kukubali hali fulani lakini semantiki inakataa.

Kwa mfano

Kuja jiana , jiwa

mfano katika sentensi

mama alijiwa na mumewe.

Kunatofauti kubwa kati ya vitenzivya asili ya kigeni na vitenzi vya asili ya kibantu ambavyo huishia

kwa irabu ‘ a’ na vya kigeni kwa u ,e , i.

**ZOEZI**

Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya kutendeana, tendea, tendwa na tendeka. Hesabu
Sadiki
Hasidi
Hujumu
Hoji
Starehe
adhimu

***This is A Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd 0746 222 000.***

**UKANUSHAJI**

Ni hali ya kubadilisha usemi Maneno au jambo kutoka hali yakinifu hadi hali ya kukana.
Ukanushaji wa nyakati na hali mbalimbali hutokea kama inavyofuata Wakati uliopo(-li)

| sentensi | ukanushaji |
|---|---|
| Alicheza jana | hakucheza jana. |
| walienda | hawakuenda |

Wakati ulipo(-na)

| sentensi | ukanushaji |
|---|---|
| Ninasoma | sisomi |

| | |
|---|---|
| Unapika | Hupiki |
| Anacheza | hachezi |

wakati ujao(-ta)

| sentensi | ukanushaji |
|---|---|
| Kitatupwa hicho | Hakitatupwa hicho |
| Ataenda dukani | Hataenda dukani |
| Embe litaoza | Embe halitaoza |

***Contact Mwalimu Consultancy 0746 222 000 / 0742 999 000 for Complete Notes.***

**HALI**

Hali timilifu (me)

Hurejelea matendo yaliotendeka muda mfupi uliopita.

| Sentensi | Ukanushaji |
|---|---|
| Alshababu wamefika kenya | Alshababu hawajafika Kenya |
| Waziri ametoa taarifa kuhusu ushambulizi | Waziri hajatoa taarifa kuhusu shabuliz |

Hali ya mazoea( hu)

Ni matukio yanayofanywa kila mara au mara kwa mara

| Sentensi | Ukanushaji |
|---|---|
| Mgaganga hugangua | Mganga hagangi |
| Wanamgambo hutatiza watu | Wanamgambo hawatatizi watu |

Hali ya (ka)

Hutumika katika vitenzi katika nyakati mbalimbali ujao, uliopita, uliopo, pia huweza kuonyesha matukio yaliyofuatana yalipotokea.

| Sentensi | Ukanushaji |
|---|---|
| Aliosha nguo akavaa, akaenda kutembea | Hakuosha nguo, hakuvaa wala hakuenda kutembea |

**Hali ya (ki)**

Hufafanua matukio yalivyotokea yakifuatana au matukio fulani yalitegemea kwa kutokea kwao, hutumiwa kuonyesha masharti

| Sentensi | Ukanushaji |
|---|---|
| Ukicheza utachafuka | Usipo cheza hutachafuka |

Hali ya- nge, -ngeli, na ngali

Hudhihirisha masharti yasiyowezakana na yanyotegemeana ambapo yale matukio ya baadaye hutegemea ya hapo awali. –nge hudhihirisha uwezokano wa kutokea kwa jambo, - ngeli na – ngali huonyesha kutowezakana kwa jambo.

| Sentensi | Ukanushaji |
|---|---|
| Ningelipwa ningemsaidia | Nisingelipwa nisingemsaidia |
| Angeliitwa ningeliitika | Nisingeli itwa nisingeliitika |
| Ungalisikiliza ungalipata Baraka | Usingalisikiza usingalipata Baraka |

*Ni nini tofauti ya kinyume na kukanusha?*

## KINYUME

Ni hali ya kupinga kwa mawazo , jambo au maana husika.

Hali ya vinyume hujidhihirisha katika kategoria tofauti tofauti kwa mfano Vinyume vya vivumishi

-baya -zuri

-fupi -refu

-eupe -eusi

Vivyume vya nomino

Mjinga mwerevu

Njaa shibe

Laana Baraka

Kitwana mjakazi

*Vinyume vya vitenzi*

*Vinyume vya hali ya kutendua*

Tega tegua

Bandika bandua

Ziba zibua

*Vinyume vya maneno yanayo kinzana*

Simama keti

Tembea kimbia

Toka rudi

Fukuza karibisha.

***Zingatia***

Iwapo vitenzivimefuatana vitenzi sambamba, basi kitenzi cha kwanza ambacho ni kitenzi kisaidizi ndicho hukanushwa.

Kwa mfano

Mama alikuwa akiwatayarishia watoto chakula

Jawabu; mama hakuwa akiwatayarishia watoto chakula.

***Huku ukitoa mifano mwafaka, tofautisha dhana zinazofuata***

Vitate

Visawe
Vitawe
Vitate
Ni maneno yanyo karibiana kimatamshi lakini yana maana tofauti sana. Mfano
Anwani –kichwa, maelezo ya sanduku la barua
Anuwai—aina tofauti tofauti
Karibia—kusongea au nusura
Karipia—kuzomea , fokea
Bacha – tundu lililoko ukutani
Pacha—vitu viwili vinavyo fanana ambavyo hutokea kwa pamoja, watoto wanao tokana kwa mimba moja.
**Vitawe**
Menono yenye maana zaidi ya moja, pia huitwa polisemia.
Kaa—aina ya mnyama wa majini, kuketi kitako , kuni ilioungua.
Chache—haribika kwa chakula au chochote kile,kuwa na hasira, chafuka kwa bahari, ongezeka.
Visawe
Ni maneno yenye maana sawa . Pia huitwa ashibahi.
Pesa, fedha ,njenje, ngwenje,
Mtu, insi, binadamu,mja, mahuluki.
Heshima, nidhamu, adabu,fahari utukufu, taadhima.
Barabara baraste njia kuu.

# UAKIFISHAJI

Ni hali inayoshughulikia alama zinazotumiwa kisarufi,huleta maana ipasavyo, kurahisisha usomaji , kuongea na hivyo neon au sentensi kufahamika vyema.
Je, matumizi ya alama za uakifishaji ni zipi?
Nukta/kitone/kituo .
Hutumiwa kuonyesha:
a) Maneno yaliofupishwa. Mfano Dkt. Mhe. S.L,P( sanduku la posta.)
b) Hutumiwa mwisho wa sentensi, kuonyesha hoja imekamilika. c) Mgao wa pesa. Mfano 70.30, ( shilingi sabini nukta na senti thelathini), 3.06( shilingi tatu na senti sita)
d) Hutumika kuandika tarehe, ambapo hutenganisha siku, mwezi na mwaka. Mfano 12.4.2016.
*Herufi kubwa H*

**Hutumika** :
a) Mwanzoni mwa sentensi.
b) Baada ya nukta au alama y a mshangao au kiulizio..hii huonyesha kwamba sentensi au maneno yanayfuata baada ya alama hizi hujitegemea hivyo huanza kwa herufi kubwa.
c) Mwanzoni mwa majina au nomino mbalimbali mfano majina ya watu, vyeo kwa kifupi,mahali miezi, siku za juma na sikukuu.
d) Kusisitiza jambo katika sentnsi mfano alitaka kujua CHANZO cha mgomo. e) Kuonyesha anwani

ya filamu, THE A HUNDREDS ,kitabu mfano GAMBA LA NYOKA.

f) Hutumika katika ufupisho wa neno au maneno mfano S.L.P, ODM, UNEP. ***herufi ndogo h***

Hutumika katika maandishi isipokuwa pale ambapo sentensi mpya inapoanzaau nomino halisi

***Ritifaa/ kibainishi ‘***

Hutumika katika uandishi wa ving’ong’o ilikuyatofautisha kimatamshi. Mfano ng’ara, ng’oa

Hutumika kuonyesha kudodoshwa kwa herufi katika neon hasaa katika mashairi. Mfano n’kaenda,’ tawasifu (nitawasifu, tutawasifu, watawasifu) *Nukta mkato/koloni/nusu/;*

a) Hutumika kutenganisha sentensi ndefu sana . Ambao huonyesha kutua au kipumuo

Nilijiuliza maswali mbalimbali, kuhusu chanzo cha yeye kuachishwa kazi; lakini sikupata jawabu, kwa sabau sikuona kosa katika utendakazi wake.

b) Hutumiwa kuunganisha sentensi mfano subira ; huvuta heri.

*Nukta pacha/ nukta mbili/koloni*

a. Hutumika kuorodhesha maneno mfano baba alimwambia alete : kalamu, vitabu, chaki na wembe.

b. Hutumiwa kutenganisha saa , dakika na sekunde. Mfano 12: 35:o4

c. Hutumika kuonyesha maneno ya msemaji badala ya kutumia alama za nukuu mfano Nilipokutana naye, nilitaka kujua ni kwanini amepote hivyo; alipenduka na kusema: nilikuwa nimtekwa nyara.

d. Hutumika kutenganisha wahusika katika tamthilia mfano

Mwelusi :naliona janga likija kwa kasi mno

Patu : lipi hilo?

e.Huweza kutanguliza kifungu kirefu ambacho kimenukuliwa kutoka kitabuni

***Alama ya mshangao/ kihisishi/alama hisi !***

Hutumiwa baada ya viigizi

Mfano tulipoenda kwao tulisikia mlio wa paka miow!

Hutumiwa kwa neon linalo onyesha hisia Fulani au mshangao. Mfano Alas ! A ajali hiyo.

***Nukta mbilina nakistari:-***

Hutumiwa kudokeza ilikutoa mifano. Kwa mfano

Ukiambiwa uoge:- tafuta sabuni, maji na kitambaa cha kutoa uchafu mwilini.

**Mkato/ mkwaju(/)**

a. Hutumika badala ya ‘au’ mfano Bi/Bw/Prof.

b. Hutumika katika nambari za kumbukumbu . mfano REF/13/07 c. Hutumikakatika kutenganisha tarehe, mwezi n siku mfano 27/1/2016.

***Nukta dukukuku …***

Hutumika kuonyesha kuwa neon lililoashwa laweza kuwa la matusi , la aibu . ni njia y kuonyesha adhabu kwa lugha

Utingo Yule alitutusi… nilishangaa sana.

Huonyesha kuwa kuna usemi au menono yaliokatwa kabla ya kukamilika. Alama za kiulizi/

kuuliza.?

Hutumika kuuliza jambo au kutaka jawabu

Mfano mbona unalia?

Hutumika kuonyesha iwapo mtu hana uhakika wa jambo au usemi fulani , hivyo hutumia alama za kiulizi

Mfano E. Kezilahabi au Mlokozi ni mwandishi wa kitabu cha GAMBA LA NYOKA?

***mabano ( )au parandesi []***

Hutumika kufungia nambari au herufi za orodha. Mfano (a) (ii)

Hutumika katika tamthilia ilikufungia maandishi ya maelekezo ya jukwaani. Mfano

Natalia :( akitembea atembea) siamini ananifanyia haya!

Hutumika kuelezea mambo fulani yasio ya lazima katika sentensi lakini huwa na maana kutegemea na muktadha husika

Alipokuwa akirudi nyumbani ,alikutana na vijana wawili( walikuwa wamshikana mikono) alijifanya hajawaona na kwenda zake.

Alama za usemi au kunukuu(‘’ ‘’)

a. Hutumika katika uandishi wa hotuba hasa mwonzo na mwisho wake. b. Hutumiwa katika usemi hasili ambapo maneno yaliyosemwa hunukuliwa.

Mfano mama alisema, ‘’ nitaenda kwenye karamu kesho ‘’.hutumika badala ya kupiga mstari chini ya neo mfano ‘’uzalendo’’

c. Hutumika wakati neno la lugha tofauti linatumiwa katika lugha tofauti Mfano tuliandaliwa ‘’indumbu’’ tulipoenda eneo la magharibi. d. Hutumiwa usisitiza maneno katika sentensi au kifungu mfano Ukija kwenye karamu hakikisha umevalia ‘’ rinda refu nyeusi’’

***Kistari kirefu – na kifupi***

i. Huonyesha kwamba neno Fulani limefika mwisho na huendelea katika mstari unaofuata.

ii. Hutumika katika uandishi wa tarehe. 12-6-2016.

iii. Hutumika kuunganisha sentensi mbili ambapo sentensi ya pili huwa ufafanuziwa sentensi ya kwanza.

iv. Mfano Haya maeneo maji hushinda yamepotea kila siku- mifereji ya kupitisha maji yalikuwa yamepasuka.

v. Hutumiwa mwanzoni mwa neno kuonyesha kuwa kunakiambishi ambacho kinahitajika. Mfano -pi? –ngineo, -eusi.

***Kipumuo/koma/mkato***

Honyesha :

a) Kupumzika kwa muda mfupi wakati wa kusoma.

b) Hutumika katika kutenganisha orodha ya vitu mbalimbali. Mfano alinunua:nyanya,vitunguu, mafuta na mboga.

c) Hutumika katika uandishi wa anwani za barua.

d) Hutenganisha sentensi ambazo zingesababisha matatizo ya kueleweka zikisomwa kwa ujumla. Mfano badala ya mamia, maelfu waliwasili. e) Hutumiwa baada ya baadhi ya vihisishi hasa

kuuliza mfano je, ni yeye kweli?
f) Hutumika katika tarakimu mfano 356,678. 120,000,05.
*Taja matumizi mengine ya alama za uakifishaji.*

## USEMI HALISI NA USEMI TAARIFA.

***Usemi halisi***
Ni maneno halisi kama yalivyosemwa na mzungumzaji. Nyakati zote hutumika, alama za kunukuu, za hisi na za kiulizi hutumika. Hutangulizwa na herufi kumbwa.
Mfano ‘’Alas! Gari limeanguka,’’Maria alishtuka.
***Usemi wa taarifa***
Huu ni usemi unaoripotiwa, ni maelezo yaliyosemwa na msemaji hutolewa maelezo tu bila kuyanukaa.wakati uliopita hutumika,alama za kuakifisha kama vile kiulizi na mshangao hazitumiki,nafasi ya tatu ndiyo inayotumiwa kwa umoja au wingi isipokuwa tu pale anayehusika msemaji.
Mfano Mwalimu alitaka kujua iwapo wanafunzi walimaliza zoezi.

**SENTENSI**
Ni mpangilio wa neno au maneno kadhaa yanayoleta maana
Kuna ina mbalimbali za sentensi

***Sentensi sahili***
Ni sentensi yenye muundo wa kishazi huru tu.
Huwa na kitenzi kimoja kikuu na huwasilisha wazo moja tu. Huchukuwa miundo miwili
a) Sentensi sahili ya kikundi tenzi pekee

***Mfano***
Analima, tuliwasili, walikaribishwa.
b) sentensi sahili ya kikundi nomino (KN) na kundi tenzi ( KT) mfano
Ongeri (KN)anasumbua( KT)
*uchambuzi wa sentensi sahili*
Analolisoma
a-kiwakilishi nafsi
na- wakati uliopo
lo-kitendwa/shamrisho
li-kiendelezi
-soma- mzizi wa kitenzi.
Faith anaimba wimbo wa taifa.
Faith ( nomino)
Anaimba ( kitenzi)
Wimbo wa taifa ( nomino)
Sentensi ambatano

Sentensi ambano ni sentensi sahili mbili au zaidi ambapo viunganishi hutumika katika kuunganisha sentensi moja na ingine . Alama za uakifishaji kama vile koma, mkato na nusu koloni hutumiwa katika sentensi za aina hii.

*Mfano*

Mama alienda nyumbani. Hakumkuta mwanawe. Alienda kumtafutaingawa hakumkuta mwanawe,alienda kumtafuta.

***Sentensi changamano***

Ni sentensi ndefu inayochanganya sentensi sahili na ambatano. Ni sentensi inayoundwa kwa kishazi kimoja huru na na kishazi kingine tegemezi sifa hii huinyeshwa kwa kuwepo kwa kirejeshi amba au –o.

*Mfano*

Askari walio uwawa huko somaia, waletwa nchini leo asubuhi , kabla ya kupelekwa makwao walifanyiwa heshima yao ya mwisho na maombi kuandaliwa katika bustani ya Uhuru.

*Sentensi huchananganuliwa kwa njia tatu kuu*

- *Visanduku*
- *Matawi*
- *Mstari.*

*Njia ya mstari*

*Mwanafunzi mtiifu atazawadiwa sare .*

*S KN+ KT*

KN N + V

N mwanafunzi

V Mtifu

KT T+KN

T atazawadiwa

KN N

N sare

Matawi

S

KN KT

N V T KN ***N***

*mwanafunzi mtiifu atazawadiwa sare.*

Visanduku

S

KN KT

. ~~N~~

Sehemu kuu za sentensi

Sentensi huwa na mkusanyiko wa maneno ambayo yamepangwa kwa utaratibu. Sehemu kuu za

sentensi ni

Kiima

Kiarifa

Kirai

Kishazi

Kundi nomino/fungu nomino( KN/FN)

Kundi tenzi/ fungu tenzi( KT/ FT)

Kiima

Ni kipasshio cha sentensi kinachodhihirisha mhusika katika usemaji. Ni nafasi inayokaliwa na kikundi nomino au nomino, pia ni mtenda katika sentensi.

**Mfano**

*Wanamgambo* walivamiwa na wanajeshi wa Kenya.

Kiima pia hupatika katika sentensi zinazo anza kwa kitenzi jina.

Mfano

*Kucheza na kuimba* kwake kunapendeza.

Kiarifa

Sehemu hii hutoa taarifa kuhusu kiima, ni sehemu ya sentensi iliyo na kitenzi. Mfano

Dada *anakimbia*

Kirai

Ni kipashio cha kimuundo kitokeacho kama nomino, kielezi au kivumishi katika sentensi.

Kuna aina mbalimbali za virai

Kirai nomino ni aina ya kirai ambapo nomino ama kiwakilishi chake ndicho hutangulia

Kira ikitenzi kitenzi ndicho hutangulia katika sentensi.

Kirai kielezi kielezi katika sentensi hutangulia

Kirai kihusishi kihusishi hutangulia kisha nomino hufuata. Kirai kivumishi katika sentensi kivumishi ndicho hutangulia.

Kishazi

Ni sehemu ya sentensi iliyo na kiima na kiarifa, vishazi huwa huru au tegemezi. Vishazi huru hujisimamia na kuwa na maana kamili ilhali vishazi tegemezi havijisimami na haitoi maana kamili, hutegemea vishazi vingine.

Kikundi nomino

Ni sehemu ya sentensi iliyona nomino au kiwakilishi chake, kivumishi, huwakisha mtenda au mtendwa, kitenzi jina . Pia huitwa kiima.

Kifungu tenzi

Ni sehemu ya sentensi inayotoa taarifa kuhusu nomino. Huwakilishwa na kitenzi au vitenzi zaidi ya moja, kielezi nomino.

# MATUMIZI YA KWA

**Hutumiwa kuonyesha nia ya neno- pamoja na**

Mfano

Vijana kwa wazee waliwasili kanisani

Kuonyesha kuwa kitu Fulani kilitumiwa kufanyia jambo Fulani Alienda kwa miguu

Alimchapa kwa mwiko.

Hutumika kuuliza maswali

Mfano

Kwa nini unapenda kusumbua?

Kwa nini unaenda?

Kuonyesha kuwa kitendo Fulani kinahusishwa na mtu Fulani

**Mfano**

Kukimbia kwa cherono kunafurahisha.

Hutumika kuonyesha jinsi jambo lilivyofanywa, litakavyo fanywa Mfano

Banati Yule alitembea kwa ujasiri.

Mtoto alioga kwa haraka iliasichelewe.

Kuonyesha sehemu ya kitu kizima

**Mfano**

Alipoulizwa mbili kwa nne hakujua.

Hutumika kuonyesha umilikaji

**Mfano**

Nitaenda kwetu

Kwangu ni kule.

Hutumika katika misemo au nahau na kwa kuunganisha maneno mawili sawa au yanayohusiana

**Mfano**

Tulionana naye ana kwa ana

Tuliandamana naye moja kwa moja hadi kwenye kituo.

***Matumizi ya ni***

Huonyesha dhana ya wingi

Mfano

Endeni

Njooni

Hutumika kama kielezi cha mahali au kuonyesha “ndani” Ameingia shimoni

Mwanafunzi aliweka vifaa vyake sandukuni. Hutumika kuelezea saa

Mfano

Ni wakati wa chajio.

Ni saa za machweo.

Hutumiwa kama vishio vya kuulizia, au viulizi Mfano

Alienda lini?

Uliambiwa nini?

Hutumika kuonyesha matokea ya vitu.

**Vitate.**

Hebu tazama maneno yafuatayo na kwa kifupi ueleze yana sifa ganiBaba papa

Ngoa ng’oa

Faa vaa

Doa ndoa

Paka baka

Kupwa kubwa

Make the highlighted letters blink

Provide space for typing in the correct answer

**Jibu**

Maneno haya yanakaribiana kimatamshi japo maana ni tofauti.Andika maana zaidi ya moja ya maneno yafuatayo:-Barabara

Ila

Provide space for learner to type in

Majibu

Barabara – Njia kuu

-Sawasawa / shwari / sawa

2. Ila - kasoro / dosari

Zoezi 4

Kamilisha methali zifuatazo

Baada ya dhiki

Mti mkuu ukigwa

Mjinga akierevuka

Kinyozi

Riziki kama ajali

Simba mwenda pole

**Faraja**

Wana wa ndege huyumba / huwa mashakani

Mwerevu yuko mashakani

Hajinyoi

Huitambui ijapo / ikija

Ndiye mla nyama

sauti, silabi na maneno

Sauti ndicho kipashio au kipengele cha chini kabisa katika lugha. Sauti hutumiwa kuunda silabi za maneno. Kwa mfano;

Maneno baba,oa na mjomba yameundwa kwa sauti zifuatazo:-

Baba ; b+a+b+a

Oa; o+a

Mjomba; m+j+o+m+b+a

Kabla ya kujenga maneno, sauti hizi hujenga silabi. Silabi ni tamko moja katika neno k.m.; Ba+ba ; = baba

; O+a; = oa

; M+jo+mba;= mjomba

; Ndwe+le; = ndwele

Kama inavyodhihirika katika mifano hii, silabi inaweza kujengwa na:-Konsonati + irabi b+aIrabi

peke yake / o/a

Konsonati peke yake m

Konsonati mbili +irabi a'mb+a

Konsonati tatu + irabi a' ndw+e

**Zoezi 3**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiambishi sahihi cha upatanisho wa kisarufi.Ulinzi mkali __tahitajika wakati wa maonyesho ya ukulima.

Marashi hayo __nanukia vizuri.

Sukari __liyopo __nawatosha nyote.

Kucheza kwa vijana wetu __liwavutia watu wengi.

Pale ndipo _lipomwagwa takataka.

Kule __nakolimwa __nahitaji kupandwa mbegu za mchicha.

Mle __nakohamia __nataka kutakaswa.

Majibu:-

Ulinzi mkali utahitajika wakati wa maonyesho ya ukulima.

Marashi hayo yananukia vizuri.

Sukari iliyopo inawatosha nyote.

Kucheza kwa vijana wetu kuliwavutia watu wengi.

Mahali ambapo panapolimwa panahitaji kupandwa mbegu ya mchicha. .Mahali ambako kunalimwa kunahitaji kupandwa mbegu za mchicha.Mahali ambamo mnalimwa mnahitaji kupandwa mbegu za mchicha.Ugali __napendwa na wakenya wengi.

**Zoezi**

Andika kulingana na maagizo yaliyo kwenye mabano

Nyumba iliyojengwa imebomoka (katika hali ya ukubwa)

Mito ile imefurika (hali ya udogo)

Kikoba kile kilichopotea kimepatikana (hali ya kawaida)

Kidole kilicho umia kimetibiwa (hali ya ukubwa)

Maduka ya rejareja yaliyofunguliwa yana bidhaa nyingi (hali ya udogo)Kiguo kilichoraruka kimeshonwa (hali ya kawaida)

Jumba lililojengwa limebomoka

Vijito vile vimefurika

Mkoba ule uliopotea umepatikana

Dole lililoumia limetibiwa

Viduka vya rejareja vilivofunguliwa vina bidhaa nyingi

Nguo iliyoraruka imeshonwa

Ngeli ya KI-V

Ngeli hii hujumuisha nomino za vitu visivyo na uhai ambazo huchukua kiambishi ki cha upatanisho wa kisarufi katika umoja na vi katika wingi .Kwa mfanoCheti kilikabidhiwa aliyefuzu

Vyeti vilikabidhiwa waliofuzu

Kijia kile kinaelekea mtoni

Vijia vile vinaelekea mitoni

Kitambulisho kilichopatikana barabarani ni cha Wafula

Vitambulisho vilivyopatikana barabarani ni vya akina Wafula.

**Zoezi**

Chagua kiambishi mwafaka ili kujaza pengo:-

Serikali itakabiliana vilivyo na ugonjwa ___naoua mifugo (a, i, u)

Serikali zitakabiliana vilivyo na magonjwa ___nayoua mifugo.(zi, ya, i)

Nyumba (umoja) ___kijengwa vizuri haibomoki. (a, i, zi)

Nyumba (wingi) ___kijengwa vizuri hazibomoki (zi, wa, ya)

Ulimi ___nawatia wengi matatani (i, u, zi)

Ndimi ___nawatia wengi matatani (zi, ya, i)

zi

## NGELI YA U-U;

Ngeli hii hujumuisha nomino zinazorejelea vitu visivyoweza kuhesabika kama vile wema, ujinga, uji, udongo. Kwa kuwa vitu hivi haviwezi kuhesabika, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi huwa U.

**Mfano**

# **POLITE NOTE!**

***Take note that this is a Sample of the Well Organized Detailed Simplified Notes.***

***Call/Text/WhatsApp 0746 222 000 / 0742 999 000 for the Complete Notes.***

# FOR MORE EDUCATIONAL RESOURCES,

# CONTACT MR ISABOKE

# *0746 222 000 / 0742 999 000*

# FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ KPLEA JOINT PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ KPLEA JOINT MOCKS
- ✓ KJSEA POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ FINAL EXAM PREDICTIONS
- ✓ KPLEA REVEALED SETS
- ✓ KPSEA EXAMS

**CALL/TEXT 0746 222 000**

mwalimuconsultancy@gmail.com

# THIS IS A PROPERTY OF MWALIMU CONSULTANCY LTD.

*Powered By Mr Isaboke*

# SUCCESS